**HOTUBA YA MHE.CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA UFUNGUZI WA KIKAO CHAAROBAINI NA MBILICHA BODI YA BARABARA MKOA(RRB) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024KATIKA UKUMBI WA RDC TAREHE 05OKTOBA, 2023.**

- ***Mwenyekiti wa CCM Mkoa,***
- ***Mwenyekiti mwenza wa Bodi ya Barabara,***
- ***Katibu Tawala Mkoa,***
- ***Kamati ya  Usalama Mkoa,***
- ***Katibu wa CCM Mkoa,***
- ***Wahe. Wakuu wa Wilaya (Sumbawanga, Nkasi na Kalambo),***
- ***Wakuu wa Seksheni na Vitengo wa Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Makatibu Tawala wa Wilaya (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),***
- ***Wahe. Wabunge,***
- ***Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,***
- ***Wahe. Wenyeviti wa Halmashauri (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),***
- ***Meneja TANROADs (M),***
- ***Meneja  wa TARURA (M),***
- ***Wakurugenzi wa Halmashauri,***
- ***Mameneja wa TARURA wa Wilaya,***
- ***Wahandisi wa Halmashauri,***
- ***Wawakilishi wa Watumiaji wa Barabara,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Wageni waalikwa,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…………..***

Awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha sisi sote kukutana kwenye kikao hiki muhimu kwa maendeleo ya Mkoa wetu wa Rukwa. Natambua kuwa miongoni mwa wajumbe na wageni waalikwa wametoka mbali na Sumbawanga, kwa kutambua hilo naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwasafirisha salama na niwakaribishe sana Sumbawanga.

***Ndugu Wajumbe,*** Kikao hiki kwangu ni cha kwanza tangu Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliponipa dhamana ya kuwatumikia Wananchi wa Rukwa. Ninamshukuru sana Mhe. Rais kwa dhamana yake hiyo kubwa ambayo amenipatia na nimuahidi kuwa sitomuangusha katika kuwatumikia Wananchi wa Rukwa. Ombi langu kwa Wanarukwa ni kunipatia ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu.

***Ndugu Wajumbe,***Kikao hiki kipo kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya Mwaka 2007 ambayo inaelekeza Kikao hiki kifanyike mara mbili kwa kila mwaka wa fedha. Sisi katika Mkoa tumekuwa tukitekeleza sheria hiyo kikamilifu kwa kuhakikisha kuwa vikao hivi vinafanyika. ambapo kwa mwaka. Nimpongeze Katibu Tawala Mkoa pamoja na wataalamu wake kwa kuhakikisha kuwa vikao hivi vinafanyika kwa mujibu wa sheria. Aidha niwapongeze ninyi Wajumbe kwa kuhudhuria kwenu kwenye vikao hivi ambavyo vimekuwa na msaada mkubwa sana kwa Wananchi wetu wa Mkoa wa Rukwa.

***Ndugu Wajumbe***,Kwa namna ya pekee nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe.**Dkt Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutupatia fedha kwaajili ya ujenzi na ukarabati wa Barabara zetu. Katika mwaka wa fedha wa **2022/2023** hadi kufikia mwezi Juni,**2023** Wakala wa Barabara TANROADs ulipatiwa jumla ya Shilingi Bilioni **10.8**kwaajili ya Matengenezo na ukarabati wa Barabara, Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 TANROADs imeidhinishiwa shilingi **Bilioni 11.9** kwaajili ya Matengenezo na Ukarabati wa Barabara. Aidha, Tunamshukuru sana Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha kwaajili ya ujenzi wa Barabara ya Ntendo – Muze –Kilyamatundu Sehemu ya Ntendo – Kizungu kwa gharama ya **shilingi Bilioni 45.3** pamoja na Barabara ya Matai – Kasesya sehemu ya Matai –Tatanda kwa gharama ya shilingi **Bilioni 37.4.** Barabara hizi zikikamilika zitainua uchumi wa Mkoa na kutuunganisha na nchi jirani Kibiashara.

Kwa upande wa TARURA hadi kufikia Mwezi Juni, 2023 Jumla ya Mikataba yenye thamani ya Shilingi **Bilioni 10.7** ilikuwa imesainiwa kwaajili ya Matengenezo ya Barabara za Vijijini na Mijini. Kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024 TARURA imeidhinishiwa shilingi **Bilioni 11.4** kwaajili ya Matengenezo ya Barabara za Mjini na Vijijini.

***Ndugu Wajumbe****,* tumekuwa na kilio cha muda mrefu kuhusu ujenzi wa uwanja wetu wa ndege wa Sumbawanga, Nitumie fursa hii kuwajulisha kuwa uwanja wetu umeanza kujengwa na Mkandarasi M/S Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd kwa gharama ya shilingi **Bilioni55.9**na Mkandarasi tayari yupo eneo la ujenzi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa

kuendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 Sura ya 2 Ibara ya 55 kuanzia ukurasa wa 71 – 78 ambayo imesisitiza uboreshaji wa Miundombinu ya usafiri.Ni imani yangu kuwa fedha hizi zilizotolewa kwaajili ya matengenezo ya Barabara na ujenzi wa Uwanja wa Ndege katika Mkoa wetu zitawanufaisha Wananchi wote, Wakandarasi wakubwa na wadogo na vikundi vya akina mama kwa kuwapa kazi za mikono (Labour based) ili kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja katika Mkoa.Katika hili ni lazima tuipongeze Serikali yetu kwani uchumi wa Wananchi wetu kwenye maeneo ya Miradi utaimarika.

***Ndugu Wajumbe,*** fedha hizi ni nyingi na Wakandarasi wazitendee haki kwa kuhakikisha kuwa miundombinu hiyo inajengwa kwa ubora.  Aidha, Viongozi wote tunalo jukumu la kuhakikisha kuwa tunasimamia kwa ukaribu miradi hiyo ili ikamilike kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa.

***Ndugu Wajumbe,***Pamoja najuhudi kubwa zinazofanywa na serikali katika kuboresha Barabara zetu bado zipo changamoto kadhaa zinazosababisha uharibifu wa Barabara zetu kama vile kupitisha mifugo kwenye Barabara, uharibifu wa mazingira unaosababisha mafuriko na hatimaye kuharibu barabara. Niwaombe viongozi wote tuliopo kwenye kikao hiki kulifanyia kazi suala la uharibifu wa Barabara ikiwa ni pamoja na kutumia sheria ndogo za Halmashauri.

***Ndugu Wajumbe***, Maendeleo haya yote yamepatikana kutokana na Mapato mbalimbali ya Serikali. Tuendelee kuwasisitiza Wananchi wetu kulipa kodi. ***UKIUZA TOA RISITI NA UKINUNUA DAI RISITI***.

***Mwisho**,* napendakutumia fursa hii kuwaomba wajumbe wote wa kikao hiki kuwa na mjadala wa kina na wa uwazi ili wataalamu wetu wanaohusika na Barabara waweze kupokea ushauri na maagizo yetu na kwenda kuyafanyia kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya Mkoa wetu wa Rukwa na Nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla.

Baada ya kusema hayo natamka kuwa kikao cha Arobaini na Mbili na cha Kwanza kwa mwaka wa fedha2023/2024cha Bodi ya Barabara kimefunguliwa rasmi.

Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA.**

Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**